OKTOBA. 2022

CHAPA YA KUMI

# TULIZO

Kwa Habari Fasaha za Fasihi



## 20 KALI ZA NINJA
JARIDA LENYE FILAMU

## KUSOMA SIACHI NG'OO
TUZO 10 ZA FASIHI ZITATOLEWA TAREHE 19 HADI 20 NOVEMBA

## NGUVU YA UPENDO
SAFARI YA MWANDISHI

## 3 KALI ZA OKTOBA

## BUINDA MJUNGU
MALKIA WA VITABU

BURE

jaridatulizo@gmail.com



# Huyu Hapa

## Buinda Mjungu

***Awali ya yote nakushukuru sana Mwandishi Frank Masai kwa kunipa nafasi kwenye jarida la TULIZO.***

Pia nakupongeza kwa wazo la kuanzisha Jarida hili.

Mimi nina majina mengi yanayotumika sehemu mbalimbali lakini kwenye ulimwengu wa USOMAJI vitabu pamoja na mitandaoni naitwa BUINDA MJUNGU.

Wengi wakiniita Malkia wa Vitabu, jina nililopewa na Mwandishi ninayemhusudu na niliyeanza kumsoma kitambo kaka Hussein Issa Tuwa.

Ni Mwajiriwa wa Serikali, Mtumishi wa Umma, mwelimishaji jamii, mhamasishaji wa masuala mbalimbali ya kimaendeleo, mfariji wa wenye huzuni na mrudisha tabasamu kwa waliyoipoteza, pia mtatuzi wa migogoro.

Ni mama wa mtoto mmoja wa kuzaa na wengi wa kulea.

Ni mzaliwa wa kwanza kati ya watoto watano katika familia. Na bahati mbaya wazazi wetu wameshafariki.

Ni mmoja kati ya waanzilishi wa taasisi ya WIWOCHI mwaka 2020 ambapo hadi sasa ipo na inafanya kazi.

Awali ilijihusisha na watoto wa mitaani, wanaofanyishwa kazi ngumu, wanaonyanyaswa na kutumikishwa kingono pamoja na wanawake (waliopo kwenye ndoa, wajane, walea peke) waliokuwa wanadhalilishwa na kufanyiwa ukatili. Ila kwa Sasa inahusika na watoto yatima na wale wasio na makazi ambapo tuna vituo sehemu mbalimbali vya kuwalea na kimojawapo kipo Jijini Arusha.

Vilevile nimefanya kazi na NGO nyingine mbalimbali zinazohusika na masuala ya Mazingira, Utawala Bora, AFYA (UKIMWI, Ujenzi wa vyoo Bora nk)

Kuhusu maisha yangu yapo rahisi, napenda KUFURAHI na kutengeneza MARAFIKI, pia kuchanganyika na watu mbalimbali. (Social Life)

***Historia kwenye Fasihi:***

Safari yangu ya USOMAJI VITABU ilianza mwaka 1989 nilipokuwa darasa la kwanza kwa kuwa mdadisi katika michoro ya gazeti la Sani ambalo alikuwa ananunua baba yangu mzazi.

Hivyo baba yangu mzazi alipoona udadisi wangu wa michoro katika gazeti hilo ndipo akaanza kunisimulia yaliyoandikwa kwenye vikatuni vya madenge, kipepe na wengineo.

Na hiyo ndio ikaleta ukaribu zaidi kati yangu na baba maana alikuwa anapenda sana kusoma magazeti na vitabu na ilikuwa kila akirudi nyumbani kutoka kazini lazima mkononi abebe Kitabu au gazeti (na magazeti ya kipindi kile

kile yalikuwa Mfanyakazi, Uhuru na mengineyo)

Baada ya kufika darasa la pili na kwa kuwa nilishajua kuunganisha maneno na kusoma sentensi nzima, nikaanza kuchukua vitabu vya baba vya Riwaya mbalimbali na kuanza kuvisoma kama vile Operesheni sukuma namba nane, Usiku wa balaa, Msako wa hayawani ikiwemo vitabu vya Waandishi Ben Mtobwa, Elvis Musiba, Sam Kitogo, Hammie Rajabu, Sam Kitogo, Eddie Ganzel, na Waandishi wengine wa kitambo.

Ila kutokana na umri wangu kuwa mdogo na aina ya vitabu nilivyokuwa nasoma kunizidi baba akataka nisome tu gazeti la Sani hadi hapo umri wangu utakaporuhusu, hivyo nikaona anaanza kunibania wakati USOMAJI ulishaanza kuniingia damuni.

Ikanibidi niwe nachukua Kitabu na kukificha kwenye madaftari na kwenda kusomea Maktaba ya Mkoa.

Kwahiyo nilianza kuingia maktaba nikiwa na umri mdogo tu na lengo nipate nafasi ya kusoma vitabu vya Riwaya kwa uhuru.

Hivyo ikabidi niwahamasishe wenzangu kwenda maktaba ili tusome na vitabu vilivyomo kule, na wakakubali hivyo nikapata kampani na ikatubidi tuwe tunatoka mapema nyumbani na kwenda huko kabla ya kuingia darasani maana masomo yalikuwa yaanza saa tano asubuhi.

Ila wenzangu wakawa wanasoma vitu rahisi tu wakati mimi nilikuwa nasoma vitu vya Kipelelezi na Kijasusi.

Na ndio Riwaya ambazo ni namba moja kwangu japokuwa na nyingine nazisoma.

Pia nasoma vitabu ambavyo ni 'non-fiction' hasa vya UONGOZI kutokana na aina ya kazi yangu.

Japokuwa kwenye USOMAJI wa Vitabu nina uchaguzi na mapendeleo yangu lakini huwa nasoma vitabu vya aina zote kutokana na jamii ninayoihudumia inahitaji mtu anayejua mambo mengi hata kama ni kidogo kidogo kwa kuwa inahitaji MTATUZI katika changamoto zao.

Baada ya hapo upatikanaji wa Vitabu ukawa unasuasua lakini yakaanza kutoka majarida kama Bongo, Ambha na Sani lenyewe (kutoka kuwa gazeti)

Pia baada ya muda yakaanza kutoka magazeti kama Kasheshe, Kiu, na yale ya Kampuni ya Global Publishers chini ya Mkurugenzi wake Eric Shigongo (ambaye naye akawa anaandika hadithi mbalimbali)

Vile vile kukaanza kuibuka vipaji vipya vya Waandishi chipukizi kama Joseph Shaluwa, Nyemo, Irene Ndauka na wenzake wa kipindi hicho, hivyo ikasaidia ule moto wa USOMAJI ndani yangu uendelee kuwaka.

Zaidi nilikuwa msomaji na mnunuzi nguli wa Vitabu na magazeti, hakuna nakala ya gazeti lolote la udaku ambalo sikununua. (Yale mengine alikuwa ananunua baba)

Kwa ununuzi huo wa magazeti ikapelekea mwaka 2009 kwenye shindano lililokuwa linaendeshwa na Global Publishers kupitia gazeti la RISASI kushinda tshirt na nikakabidhiwa na Wakala wao wa Arusha.

Hivyo tangia nimeanza kupenda USOMAJI wa Vitabu hadi sasa nimesoma vitabu vingi na kufahamiana na Waandishi wengi.

Pia imenisaidia kupata MAARIFA mbalimbali, na kwakuwa kujifunza hakuna mwisho ndio maana sichoki kusoma vitabu.

Na kwa kuwa nimeanza kusoma vitabu siku nyingi karibia miaka 32 sasa, hata USOMAJI wangu vitabu ni tofauti kwa maana ya kuweza kusoma zaidi ya vitabu 100 kwa mwaka. (Kwamba kila siku lazima nisome, na kila ninapokuwepo lazima nisome)



Pia nafurahi kwa kuwa sasa hivi Waandishi ni wengi, na vitabu vya kusoma ni vingi, na zaidi ulimwengu wa teknolojia umerahisisha sana upatikanaji wa Vitabu hasa kwa "soft copy"kwamba unaweza kusoma kupitia simu yako ya mkononi.

**CHANGAMOTO:**

*- Baadhi ya Waandishi kuchapa vitabu vichache kwa oda hivyo kukosekana kwenye soko pale mtu anapohitaji.*

*- Baadhi ya Waandishi kutokuwa waaminifu (kupokea hela ya mteja na kutokomea nayo)*

*Gharama kubwa za usafiri hasa kwa vitabu visivyopatikana mikoani*

**USHAURI:**

*- Waandishi wajitahidi vitabu vipatikane ili wapatikane WASOMAJI wengi wapya*

*- Vitabu vitangazwe kwa kutumia platform mbalimbali ili watu wajue uwepo wake sokoni*

*- Kuwe na Umoja Imara wa Waandishi kama kulivyo na Chama cha Wafanyakazi, Walimu, Madaktari nk*

*- Kuwepo na MSHIKAMANO na ushirikiano kati ya Waandishi na WASOMAJI.*

*- WASOMAJI wanaojitoa kwa ajili ya Fasihi wathaminike na kupewa Moyo maana mara nyingi kazi wanayofanya ni ya kujitolea.*

**Ahsanteni, na Mungu awabariki Waandishi wote!**

# ZULIA LA FASIHI






## 20 KALI ZA NINJA

### *Hatua Mpya ya Fasihi*

Ni mwezi ambao ulikuwa na mashamushamu ya kila aina. Nazungumzia mwezi wa kumi ambao uligubikwa na tukio la uzinduzi wa kitabu cha kwanza ambacho kimejazwa filamu ishirini. Ndio, ni ishirini kali za ninja ambacho kimeandikwa naye Bwana Kaisal Ally.

Ishirini kali za ninja, kiliweza kupata wasaa wa kuzinduliwa Manzese, Dar es Salaam na kuhudhuriwa na wanafasihi kedekede kama vile Kado Cool, Hussein Molito, George Mosenya, Abyas Mzigua na wengine wengi huku wadau mbalimbali pia wakijitokeza kuunga mkono tukio hili. Watu kama Ney Aron, Gervas, David Shalali, Yusta Lucas walipamba tukio hili la kihistoria. Tulizo Media pia tulikuwepo na tulishuhudia tukio hili likifana.

Mwandishi Kaisal ameweza kuthibitishia uma kuwa kila kitu kinawezekana kwa kalamu. Kwani badala ya kuchambua filamu kwa njia ya sauti au video, yeye kaandaa kitabu ambacho kimejaa uchambuzi wa kuvutia. Hii ni hatua mpya katika fasihi ambayo kijana huyu kaweza kuipiga.

Wapo ambao wanaendelea kuikuza fasihi yetu kwa kila njia lakini Kaisal yeye kaweza kupita kwenye njia ambazo kwake zimemwingiza katika kitabu cha kumbukumbu bora za kifasihi. Tulizo Media, tunamtakia Kaisal kila la heri katika hatua hii mpya ya kifasihi.

# TUZO ZA 10 FASIHI YA KISWAHILI KUTOLEWA KWA WANAFUNZI NA WADAU WA FASIHI TANZANIA.







## NA MWANDISHI WETU

Tuzo za umahiri katika uandishi wa fasihi ya Kiswahili zinatarajiwa kutolewa Novemba 19 mwaka huu katika Tamasha la pili la Fasihi ya Kiswahili nchini linalotarajiwa kufanyika Kisarawe mwaka huu.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Mratibu wa Tamasha la pili la Fasihi ya Kiswahili, Goima Mwamwingila, inasema kuwa tuzo hizo za fasihi ya Kiswahili ya Taffu zitatolewa kwa wanafunzi 6 wa shule za msingi na Sekondari, pamoja na wadau wengine waliofanya vizuri katika Sanaa ya Fasihi.

"Wapo watu wengi nje ya wanafunzi hawa wanaostahili tuzo ambapo sisi TAFF tutawatunia wachache wake ikiwemo wengine ambao wameshatangulia mbele ya haki!" Alisema Mwamwingila na kuongeza kuwa Tamasha la Fasihi ni kwa kila mmoja na wanafasihi wote wanaalikwa kwenda kushiriki Tamasha hilo.

Alisema Tamasha la mwaka huu linatarajia kupata wageni kutoka nchini Ghana, Nigeria na Kenya na litafanyika kwa siku mbili tofauti na Tamasha la mwaka 2021 ambalo lilifanyika kwa siku moja.

"Tamasha la pili la Fasihi ya Kiswahili litafanyika kuanzia tarehe 19 na 20 katika ***Uwanja wa wazi wa Chanzige Sekodari*** ndani ya ***Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe mkoani Pwan***i, ikiwa na kauli mbiu ya ***'KITABU KIMA MAHALI - KUSOMA, SIACHI NG'O!'*** " Ilisema taarifa hiyo

Mwamwingila aliongeza kuwa wadau mbalimbali wa akiwemo Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa wamealikwa na na wanatarajiwa kushiriki.

Alisema wadau wengine walioalikwa ni pamoja na **Baraza la Sanaa la Taifa (Basata)**, *Chama Cha Hakimiliki (COSOTA), idara ya Kiswahili na Sanaa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Baraza la Kiswahili la Zanzibar (BAKIZA)* na *Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA),* Wanafunzi wa Shule Sekondari, *Ofisi ya Mbunge Kisarawe, Mkuu wa wilaya* na wadau wengine wa fasihi.

Mratibu huyo wa Tamasha alisema Tamasha hilo linalofanyika mara moja kila mwaka lina malengo kadhaa mojawapo likiwa ni kuwaleta pamoja wadau wa fasihi na jamii ili kujadili namna bora ya kuifanya fasihi kuwa zana muhimu ya maendeleo ya jamii.

Alisema Tamasha linalenga kurejesha ari ya Jamii kupenda kusoma vitabu ikiwa ni pamoja na kujenga uwezo kwa watunzi wa kazi za kubuni, kubuni kazi za fasihi zenye tija na maslahi kwa jamii zao.

Mwamwingila alisema, malengo mengine ni kutoa tuzo za umahiri kwa kazi za fasihi ya Kiswahili zilizozofanya vizuri mwaka 2022 kwa wanafunzi wa Shule za Msingi na Sekondari, kufanya uzinduzi wa vitabu viwili vya hadithi za wanafunzi walioshinda mwaka 2021 na kufanya maonyesho na mauzo ya vitabu.

Alisema, Tamasha litatumika pia kuchangia vitabu kwa ajili ya maktaba ya Shule ya Msingi na Sekondari, kuzindua riwaya za aina mbalimbali, kufanya utalii wa kifasihi katika eneo la ushoroba na kuwakumbuka wanafasihi waliofanya kazi iliyotukuka ambao kwa sasa wametangulia mbele ya haki.

Alitoa wito kwa makampuni ya kibiashara na wadau wengine kujitokeza kudhamini shughuli mbalimbali za Tamasha hilo ili kupata fursa ya kujitangaza na kuuza bidhaa zao kwa kuwa Tamasha linatarajia kukutanisha wadau zaidi ya 500 wa fasihi kutoka Tanzania na nchi kadhaa




za kiafrika.

Alisema Tamasha linatarajiwa kufanya mjadala wa kitaifa kuhusu ukuzaji wa Kiswahili na fasihi ambapo jumla ya mada tano zitajadiliwa na kuwekewa maazimio.

"*Mada Kuu ya mwaka huu ni "**KITABU KILA MAHALI – KUSOMA SIACHI NGO!*** Lengo la mada hii ni kuendeleza kampeni ya mwaka jana iliyokuwa na kauli mbiu ya kusoma siachi ng'o hivyo mwaka huu wanataka kuona vitabu vnapatiaka zaidi!" Alisema Mwamwingila na kuongeza kwamba mada zingine ni pamoja na; Wajibu wa Wazazi/Walezi/Walimu kujenga Tabia ya Usomaji wa Vitabu kwa watoto, vijana na watu wazima; Nafasi ya Wanawake na wasichana katika Fasihi kama watunzi, Walezi na Wazazi; Nguvu ya Fasihi katika kudumisha/Kuendeleza Amani; TEKNOHAMA, Fasihi na Maendeleo ya Watunzi pamoja na Nguvu ya Umoja katika kuinua Fasihi Andishi.

Tamasha la Fasihi ya Kiswahili huandaliwa kila mwaka na Taasisi ya Tanzania Fasihi Fund (TAFF) iliyopo Kisarawe, kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa fasihi ikiwemo Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe mkoani Pwani.












# SAFARI YA MTUNZI

> ***"Nilianza na Fasihi Simulizi kabla ya kuingia katika Fasihi Andishi."***
>
> **Erick Mbise**

Mimi naitwa Erick Mbise ni mzaliwa wa Arusha, Tanzania. Bila kupoteza wakati napenda nikupitishe kidogo katika safari yangu ya uandishi wa vitabu. Naweza kusema nilianza na Fasihi simulizi kabla ya kuingia katika Fasihi andishi. Nilipokuwa shule ya msingi Songoro nilipenda sana kusimulia hadithi kwa wenzangu. Baada ya masomo ule muda wa mchana kuanzia saa Saba waalimu walikuwa hawaingii katika vipindi hivyo nilikuwa napata wasaa wa kuwaketisha wenzangu kitako na kuwapa hadithi. Nilijipatia umaarufu katika hiyo hali na muda mwingi nilizungukwa na kundi la wanafunzi kusikiliza hadithi. Katika hatua hii nilipitia changamoto moja kubwa ambayo ilikuwa ni lugha ya Kiswahili kwani alifika mwanafunzi mgeni aliyekuwa anaitwa Michael, yeye alikuwa hajui Kimeru na mimi sikujua kuongea Kiswahili vizuri. Hivyo akitaka kuja kupata hadithi kwangu nilikuwa namkimbia kukwepa kuongea Kiswahili.

Nilivyoanza sekondari nilipenda sana kusoma vitabu vya hadithi. Nilikuwa nalala hadi saa nane usiku kwa ajili ya kusoma vitabu vya hadithi.

Nakumbuka nilivyoanza kidato cha tano nilianza kuandika stori katika karatasi kisha nikawa naziweka sehemu moja. Baadhi ya wanafunzi wenzangu waliosoma stori zile walivutiwa sana na kwa kipindi hicho nilikuwa naandika kwa lugha ya Kiingereza. Japokuwa nilikuwa naandika lakini nilikuwa sijapata wazo la kuandika kitabu hivyo hata zile karatasi zilipotea.

Mwaka 2018 nikiwa nasoma Chuo kikuu cha Dodoma (UDOM) nilipata msukumo wa kuanza kuandika na nikawa napata shauku ya kuwa na kitabu. Nilianza kutafuta wazo la kuandika na nilipata wazo la kuandika kitabu kuhusu Furaha. Sababu kubwa iliyonifanya kuandika kuhusu Furaha ilitokana na maisha yangu ambayo nilipitia ya kukosa furaha kipindi nikiomba mkopo wa masomo ya chuo kikuu na masuala ya kutafuta chuo. Nilikuwa nimepitia majarida mbalimbali yanayohusu furaha lakini nilipitia pia vitabu na kujifunza juu ya furaha. Hivyo nilichagua wazo la kuandika kuhusu Furaha kwa sababu niliamini ingekuwa rahisi kwangu. Baada ya muda nilikamilisha kwa kiasi ambacho niliweza.

Nilifurahi sana nilivyokamilisha kile kitabu lakini sikuwa najua chochote kuhusu uchapishaji wa vitabu. Baada ya kutafuta kwa muda nilikutana na Dickson ambaye alikuwa anafanya kazi ***stationary*** moja karibu na chuo akaniambia anaweza kunitengenezea jalada la kitabu na kuchapa kitabu. Alimaliza kazi ya kutengeneza jalada la kitabu na alifanya vizuri. Ilipofika kipengele cha kuchapa aliomba kukagua kitabu. Bahati nzuri alikuwa msomaji wa vitabu hivyo alibaini makosa mengi na alinirudisha na kitabu akaniambia nikatulie nirekebishe nibadili na jina la kitabu hivyo hakikuitwa tena **FURAHA YANGU** kikaitwa **ITAMBUE FURAHA**. Sikuchukia nilirudi nikabadili nikapeleka tena kwa ajili ya kuchapa.



Kwa kipindi kile sikuwa na fedha nyingi hivyo nilimuomba anichapishie nakala tano tu. Sikuwa na uzinduzi zaidi ya kurudi na kuweka ***status WhatsApp***. Nashukuru wengi walinipokea vizuri na wachache walitamani kupata nakala. Nilipoangalia ndani ya kitabu nilibaini tena makosa tena mengi hivyo sikuuza tena vile vitabu vitano ilinibidi nihariri tena. Nilisubiri mpaka hela ya mkopo wa Chuo itoke ndipo nichape tena nakala nyingine. Nilivyopata hela kweli nilichapia vitabu pale ***stationary*** kwa Dickson japo mwonekano wa kitabu haukuwa mzuri maana ile kazi ilifanyika kwa vifaa vya kawaida.

Tulikata kawaida ikawa na mwonekano kama imekatwa na panga, lakini pia mkunjo wa kitabu haukuwa vizuri hivyo ikawa kama kitini.

Niliuza vile vitabu lakini nilijaribu kuandika stori na nilianza kwa kuweka status WhatsApp. Watu wengi walinipokea vizuri sana kila mtu akawa anatamani kupata mwendelezo wa hadithi. Hapo ndipo nilipoamua kuanza rasmi kuandika riwaya. Nilivyoanza kuandika riwaya nilibahatika pia kupata mchapishaji kutoka Morogoro ambaye alichapa kitabu changu cha kwanza cha riwaya kilichoitwa **SITAKUACHA OBADIA**. Kazi ilikuwa nzuri na tayari nilikuwa nimepata mwangaza wa kazi hivyo kilihaririwa pia na rafiki yangu ambaye alikuwa anasoma masuala ya Fasihi na uhariri (UDSM) alikuwa anaitwa Gift Nnko.

Niliendelea na uandishi nikaandika kitabu cha tatu **SANDUKU JEUSI**. Hiki kitabu nilitamani kuzindua na nilialika marafiki ila waliofika walikuwa watano na walikuwa wale marafiki zangu wakiume tu. Nilizindulia sehemu inaitwa Ziwa Duluti na hela nilizopata kwenye uzinduzi nakumbuka tulinunulia ugali na nyama hivyo sikurudi nyumbani na hela yoyote ya uzinduzi. Kwa hapo lengo langu halikuwa hela ila kutangaza kitabu. Kitabu cha nne kilikuwa ni **NITAKUONA TENA** nilibahatika pia kuzindua angalau idadi ya watu waliongezeka hadi kufika kumi hapo wakiwemo vijana wa kiume na kike.

Kwa sasa hivi nipo katika maandalizi ya kutoa kitabu cha tano ambacho kitakuwa katika lugha ya Kiswahili na Kiingereza na kimehaririwa na mtu anayejua hiyo kazi ya uhariri. Pia nina vitabu vingine vikiwemo vitabu vya maarifa na mojawapo ni kitabu kinaitwa KIJANA NJE YA MWENENDO ambacho nilianza kuandika 2019 hadi sasa 2022 naendelea nacho maana kinahitaji tafiti za kisayansi. Kitabu kinagusia masuala ya utoaji mimba, madawa ya kulevya na Punyeto kwa wanaume. Kuchelewa kwake inasababishwa na kuhitaji tafiti nyingi kutoka kwa wahusika ili kuja na kitabu ambacho kimekamilika.

***Changamoto zipo nyingi katika uandishi na miongoni mwa hizo changamoto ni,***

Kupata muda wa kuandika, Kwa kipindi cha nyuma nilikuwa nasoma hivyo ilikuwa inanibidi kupunguza muda wa kujisomea kwa ajili ya uandishi. Kuna wakati nilikuwa nalala saa saba usiku kwa ajili ya kitabu. Lakini kwa sasa hivi ninafanya kazi mbalimbali kama biashara na ajira ya ualimu katika shule ya walemavu hivyo napata muda mchache wa kutulia na kuandika.

Changamoto ya fedha, hii ilikuwa kubwa zaidi kipindi cha nyuma. ilinibidi kutumia hela ya matumizi kwa ajili ya vitabu. Lakini pia kwa sasa hivi changamoto ni kupata fedha kwa ajili ya kufanya kazi na watu wazoefu kama wahariri ambao baadhi yao gharama zipo juu ukilinganisha na kiasi ninachopata katika mauzo.

Soko la vitabu, Bado soko la vitabu lipo chini kutokana na watu wengi kutokupenda kusoma vitabu. Lakini pia sijaweza kutengeneza namna nzuri ya kuuza vitabu mpaka sasa hivi nina wakala mmoja ambaye yupo Arusha mjini ananiuzia vitabu kisha anachukua asilimia fulani ya mauzo.

Baadhi ya changamoto nimejaribu kuzifanyia kazi kama kutafuta watu wanaofanya kazi katika tasnia ya uandishi na wamekuwa washauri wazuri na kupata kazi nzuri zenye ubora akiwemo Frank Masai mmiliki wa Tulizo Media, Hassan Mboneche, Stallone Joyful na wengine ambao sijawataja kwa majina.

kutumia mitandao ya kijamii kama Facebook, Instagram na WhatsApp katika kutangaza biashara zangu za vitabu na imekuwa njia nzuri na yenye tija katika soko na kujitangaza.

**MALENGO**

Malengo yangu makubwa ni kuuza vitabu dunia nzima na tayari nimeshaanza mchakato. Nimefanikiwa kuuza vitabu Ujerumani na Marekani kupitia marafiki ambao ninakutana nao katika kazi yangu ninayofanya. Katika kuhakikisha naifikia Dunia nzima kwa vitabu vyangu nimeanza kutoa vitabu katika lugha ya Kiswahili na Kiingereza. Mapokeo kwa marafiki wa nje ya nchi ni mazuri wanapenda





kusoma hivyo hutumia hata aplikesheni kwa ajili ya kusoma kutoka Kiswahili kwenda Kiingereza na wanapenda pia kusoma vitabu vya Kiswahili kama sehemu ya kujifunza lugha ya Kiswahili.

Kutengeneza mfumo mzuri wa uuzaji wa vitabu na tayari kwa vitabu vya mafundisho. Nimekuwa nikialikwa sehemu mbalimbali kama makanisani kufundisha somo la furaha hivyo kuuza nakala na maarifa yaliyopo kuwafikia watu wengi.


Mapokeo kwa familia yangu naweza kusema siyo mabaya wala siyo mazuri sana. Hawapingani na ninachofanya lakini siyo wafuatiliaji wa kazi zangu sana na hii ni kutokana na tabia ya kutokupenda kusoma hivyo siwalaumu. Bado nazidi kuwashawishi kupenda kusoma na mwitikio umeanza kuonekana.

**MWISHO**

Nipende kutoa shukrani zangu za dhati kwa Jarida la Tulizo kunipa nafasi ya kujitambulisha. Lakini pia watu wote ambao wamekuwa wakinishika mkono katika kazi zangu za uandishi. Karibu ujipatie nakala za Erick Mbise.


*Mawasiliano: 0764016589*
*Email: mbiseerick4@gmail.com*






# WAZO LA MWANDISHI



## Nguvu Ya Upendo

Na Xavery Luoga

***Kumbato la mama, lanifikisha mwaka 2018, nikiwa nawaza namna ya kutengeneza kitabu kimoja kizuri cha kuvutia, na ndipo safari ya Nguvu ya Upendo ikaanza.***

***Hapo kabla, Sikuwaza kama Nguvu ya Upendo inaweza kuninufaisha na kuniliwaza hata nyakati ngumu. Asante mungu nimeweza.***

***Hadithi yake niliitunga nikiwa na akili timamu, nikiwa tayari nimeshaonja joto la dhuluma wafanyalo baadhi ya Wamajuu kwa kulaghai baadhi ya kazi za waandishi wachanga kisha kuchomoka na kitita kilichotumika kama imani ya mwandishi kwake. Hehe, nimeionja hiyo, lakini kwenye mkasa mwingine wa kitabu ambacho bado hakijatoka, mkasa ambao nikipata muda, basi nitauweka wazi rasmi ukiwa na ushindi mnono wa kitabu chake.***

Nikiongelea RIWAYA: *NGUVU YA UPENDO*, msingi wake ulianzia katika wazo la kumuongelea mwanamke kwa namna chanya; kama binadamu ambaye anapaswa kuwa na misingi na malengo yake kwa kujiongoza na kuwa na nguvu katika jamii.

Nafasi ya mwanamke katika jamii, ndio haswa mlengwa wa kazi yangu. Ni kwa namna ambavyo napaswa kumuibua mwanamke kutoka katika wimbi la manyanyaso kifikra, kiuchumi, kijamii, kitamaduni, kisiasa na mambo mengine mfanano na hayo, kwa kutumia mhusika mwanaume atakayepambana kwa ajili yake, na pia kumtumia mwanamke yeye kipinga masuala kama; Kuchaguliwa Mwenza, Kulazimishwa kuoa, kunyamazishwa kuzungumza, kuwa chini ya mabavu ya mwanaume, kuaminika katika uongozi na kadhalika. Nilipokua naandika, nimeegemea zaidi katika nafasi hiyo.

Kazi ilikuwa katika mtindo wa masimulizi ikiwa na Jina la PENDO HURU kisha kuanza kuruka kwa uchache huku Facebook kabla wazo wa Kitabu halijanijia. Wazo la kuweka katika mfumo wa kitabu, lilianzia pale ambapo, Simulizi ya PENDO HURU ilipoibuka kidedea –namba moja, katika Tuzo za Mwandishi Bora, zilianzishwa kwa mara ya kwanza, ikichuana na riwaya nyingine bora kutoka kwa waandishi ambao nilikuja kuwafahamu kupitia shindano hilo.

Pesa za Uchapaji wa Kitabu, nilizipata kupitia kiinua mgongo cha bodi ya mikopo, ambapo nilijikopesha mimi mwenyewe kwenye kitabu, na kuapa kujilipa baada ya mauzo.

Sitaki kusema kuwa nilipata mtelezo katika uchapaji, No! ila ni kwa sababu nilishafahamu wapi napata huduma nzuri, kwa bei nafuu na kwa uhakika zaidi. Kwani nyoka wa kijani alishaniondoka na kisogo cha mguu wangu kwenye wazo la kitabu cha kwanza, hivyo nilikimbia kila rangi ya kijani yenye mfanano wa nyoka huyo. Hussein Molito kupitia, Molito Brand na Kalamu Tulivu, alifanikiwa kunipokea kwa mikono miwili, mimi na kazi yangu!, kwa ugumu uleule na uandishi uleule, nikafanikiwa kutoa kitabu na kutibu ile hulka ya siku moja nami nitamiliki ktabu changu.
Frank Masai, nae kwa wakati wake, alinifanikishia kuchapa nakala ya pili ya NGUVU YA UPENDO ikiwa na mwonekano mpya katika jalada na mpangilio wa ndani.

Ya Mungu hayana mipaka, Kazi inanifanikisha kwa mengi sana, nilifanikiwa kuuza nakala zaidi ya 200, kwa wakati tofauti, kwenye mikoa kama Arusha, Tanga, Iringa, Kilimanjaro, Zanzibar, Songea na Dar es Salaam.

Kuanzia hapo, nikafahamika zaidi na watu, si watu tu; bali ni watu wa maana ambao wengi sikuwahi tarajia kama nitakuja kukutana nao kirahisi. Tena wengine kunipa hadi jina la Mkandarasi.




Bado nafaidi matunda ya kitabu cha NGUVU YA UPENDO kwa mwaka mmoja sasa. Na kinanipa chachu ya kuendelea kutoa vitabu vingine lukuki bila kuchoka.

Kitabu kinapatikana katika mfumo wa nakala ngumu kwa Tsh. 10,000/=, na nakala tepe kwa 5,000/=, kwa mawasiliano ya 0672493994 popote pale.

Katika shukrani, Mungu wa Kwanza, pia;
Ahsante tena mama, kwa baraka zako za mikono miwili katika shughuli zangu za uandishi.
Ahsante sana kwa Simulizi Huru Media Production chini ya Sam Darfur, kwa kuniunga mkono nyakati zote niwapo ndani na nje ya kundi.
Ahsante sana, Molito na Frank kwa kuamini kuwa naweza fika mjini na kunipa chachu ya Mwandishi kuwekeza katika vitabu.
Ahsante shabiki zangu wote, kwa sapoti zenu muhimu kwangu.
Haijalishi nimeteleza mara ngapi, nguvu za kuanguka bado zipo.. twen'zetu.

Xavery Emmanuel Luoga (Mkandarasi)
WhatsApp +255672493994
Xavemmanuel12@gmail.com




**TULIZO MEDIA**

TUNATOA HUDUMA KAMA VILE

- Kuchapa Vitabu
- Graphics & Design
- Uhariri
-Uhakiki
- Ghost Writing
-Kutoa Ushauri wa Kiuandishi
-Kuandaa Simulizi Za Sauti
- Kutengeneza
i)Mpango wa Biashara (Business Plan)
ii)Mpango Kazi (Project Proposal)

MAWASILIANO
*tulizomedia@gmail.com*
*tulizographics@gmail.com*
*jaridatulizo@gmail.com*

*+255 627 585 638*
*+255 752 353 039*

KARIBUNI SANA








# MSOMAJI WETU

## KASSIM NANGALE

***Mwezi wa Oktoba, Tulizo tulipata nafasi ya kukutana na msomaji mwingine ambaye kwa sasa kaweka makazi yake katika huko Geita. Kama kawaida yetu tulimtwanga maswali kadhaa ya kimaisha na uandishi kwa ujumla.***

***Kassim Nangale anasimama hapa kama msomaji wa vitabu na hadithi kwa ujumla Na haya ni sehemu ya mazungumzo yetu.***

***1. Jina lako ni nani? Je, una watoto wangapi? Je, umeoa?***

Naitwa Kassim Mustapha Nangale, Ni Baba wa Familia ya Mke mmoja na Mtoto mmoja wa Kike, Christina. Ni mwajiriwa Wa Serikali na ninaishi Mkoani Geita.

***2. Ilikuwaje ukaingia kwenye usomaji wa vitabu?***

Ilitokea Tu nikajikuta napenda kusoma Vitabu. Mwanzoni nilianza Kwa kusoma katuni magazetini hasa gazeti la Sani. Vile vituko vya Zena na Betina, Bush stars nk. Pia waandishi kama Sultan Tamba, Irene Mwamfupe Ndauka, Eric Shigongo, Zubagy Akilimia, walinivutia kusoma hadithi. Nikiwa mdogo kabisa nilikua nauza fagio, makopo ya Shaba maarufu kama "Siso" na nikipata pesa nilikua naenda kununua majarida ya Zubagy Akilimia na Irene Mwamfupe pale Feri nje na Soko la Samaki. Nakumbuka ilikuwa miaka ya 2003 au 2004 hivi. Baadae ndio nikaanza kusoma Vitabu vya Erick Shigongo. Kitabu kama "Rais Anampenda Mke wangu", "Machozi Jasho na Damu," ni Vitabu vyangu vya awali kabisa kuvisoma.

***3. Ukiwa mtoto wazazi wako wamewahi kukununulia vitabu?***

Wazazi wangu Kiukweli kabisa hawakuwahi kabisa kuninunulia Kitabu zaidi Baba alikuwa na vitabu kadhaa vya Chama cha Mapinduzi. Vitabu vyake vingi vilikua ni Mambo hayo ya Chama na Kwa kifupi wazazi wangu si wapenzi Sana Wa kusoma Vitabu.

***4. Kwa mwaka unanunua wastani wa vitabu vingapi?***

Kwa Mwaka ninanunua Vitabu zaidi ya nakala kumi Kwa ajili ya familia Yangu. Mfano Mwaka huu nimemnunulia Binti Yangu zaidi ya Vitabu sita Kwa ajili ya kujisomea. Miongoni mwa hivyo Vitabu nimemuwekea na Kitabu cha "KIBEKA" kilichoandikwa na Muddy Mwanaharakati ili aanze kuzoea kusoma riwaya na namuona ana mwelekeo mzuri.

***5.Unasoma vitabu vingapi kwa mwaka?***

Binafsi huwa Nina uwezo wa kusoma zaidi ya vitabu 8 Hadi 10 kwa mwaka. Ila huwa nina kawaida ya kuzipa kipaumbele na kuzirudia zile riwaya ambazo nakuwa nimezipenda. Unajua usomaji wa riwaya ni ulevi, kwa hiyo kuna muda unajikuta hata kama una kitabu kipya mkononi, ukakumbuka kitabu fulani unajikuta umekirudia. Pia ili usome na umuelewe mwandishi huwa naamini kuna ulazima wa kukirudia kitabu zaidi ya mara moja.

***6. Kitu gani unatamani sana kitokee kwenye tasnia ya vitabu?***

Kiukweli natamani siku moja kuona Filamu zinazotokana na waandishi wa Riwaya. Kuna Riwaya zina mafunzo makubwa mno kwa jamii lakini kutokana na kwamba sio watu wote katika jamii wana tabia ya kufukua yaliyofukiwa kwenye vitabu wanajikuta hawajifunzi. Ukisoma Kitabu kama MWIMBULA kuna

funzo kubwa mno kwa wale wote wanaohisi wanateswa na ndoa zao. Lakini leo hii unaweza kwenda kuulizia watu 10 kwenye jamii basi ni mmoja au wawili ndio wanaweza kuwa na ufahamu kuhusu kilichoandikwa kwenye kile kitabu. Tofauti kabisa na ukilinganisha na Filamu. Ingawa hapa najua changamoto ni mtaji, ila soko lipo kubwa mno.

***7. Una mpango wa kuandika kitabu?***

Kuandika Kitabu sijawa na mpango huo kabisa ingawa huwa napenda sana kuandika Script fupifupi sana upande wa maigizo. Nilikua naandika vipande vifupifupi vya hadithi toka nikiwa Shule ya Msingi, Sekondari na hata Leo kazini sijajitenga sana na kazi za sanaa ila uandishi wa kitabu sijawaza. Labda baadaye huko Mungu akijaaliwa naweza andika Historia ya Maisha Yangu maana nina mengi Sana ya kuwashirikisha Walimwengu ambayo wanaweza kujifunza na kuelimika kupitia mimi.

***8.Vitabu gani bado vinakuvutia hasa hivi vya kuanzia miaka ya 2000?***

Vitabu vya miaka 2000 ambavyo bado vinanivutia hata Leo ni *Tutarudi na Roho zetu Cha Musiba, Machozi Jasho na Damu cha Erick Shigongo.* Lakini pia kuna *Uchawi wa Mchungaji Stephano* kiliandikwa na *Irene Mwamfupe Ndauka.*

***9. Ungekuwa sehemu ya serikali, ungeifanyia nini tasnia ya uandishishi?***

Kikubwa ambacho ningekifanya au natamani wenye mamlaka wakifanye ni kuhakikisha waandishi wanakua na jukwaa lao. Kuwasaidia upatikanaji wa hakimiliki ya kazi zao. Lakini kutumia kazi zao kwenye mitaala ya elimu kuanzia Elimu ya Awali hadi vyuo vikuu. Kwa sasa waandishi wamegawanyika sana na wapo makundi. Lakini waandishi ni jeshi kubwa mno lenye nguvu ya kufanya mageuzi ya aina yoyote kwenye jamii bila Kujali ni mageuzi hasi au chanya..

***10. Unawaambia nini wasomaji wengine?***

Nikiwa kama mdau wa kusoma Vitabu nazidi kuwakumbusha wasomaji wenzangu wajitahidi kuwaunga mkono waandishi kwa kununua kazi zao kwao wenyewe au kwa mawakala wao. Watoe taarifa pale wanapoona wizi au unyonyaji wa kazi za mwandishi. Mfano siku hizi Kumekuwa na wimbi kubwa la wasambazaji holela wa kazi za waandishi Kwa mfumo wa nakala laini. Msomaji makini na anayejali kazi za mwandishi hawezi kukubali kununua nakala laini kiholela na kuacha kununua Kitabu Kwa mwandishi husika au Wakala wake. Jukwaa la pamoja la wasanii ndio suluhisho la kuwaleta pamoja waandishi ktk kupigania na kutetea maslahi yo. Mpaka sasa kazi waliyofanya waandishi ni kubwa lakini si sawa na kile wanachokivuna. Nitoe Rai Yangu pia Kwa waandishi waandamizi kama Hussein Tuwa, Mzee Beka Mfaume, Erick Shigongo nk Wanayo nafasi kubwa Sana ya kufanya jambo kwa ajili ya kuwaongoza vema waandishi kama Patrick Ck, Frank Masai, Hussein Molito, Japhet Nyang'oro, Maundu Mwingizi, Laura Petie, Bahati Mwamba, Fathy Mtanga, Salim Ng'anzi nk Kwa kuwa na Chama kimoja cha waandishi chenye Nguvu.

Lakini Pia ninatoa pongezi Kwa aliyeanzisha ule uwanja wa "Kona ya Riwaya" na baadaye "Kona ya Riwaya reloaded" pale Facebook hakika alijua kutuleta pamoja na kutufanya tufurahie kazi za waandishi wetu!!



# TATU KIONDO KUTOKA KUANDIKA HADI KUWA MJASIRIAMALI

Naitwa Tatu Kiondo, nina miaka 30, sijaolewa nina mtoto mmoja.

Nilikuwa na biashara ya saluni ambayo niliacha muda kidogo. Kwa sasa nimejikita kwenye biashara ya kuuza mashuka kupitia Tatians Store.Biashara hii ina miezi kama mitatu.

Ili ukue kibiashara lazima ukutane na changamoto za hapa na pale mimi binafsi huwa napambana nazo hasa mfano mteja amekuagiza shuka umpelekee mnapanga kukutana labda kituoni basi ukifika muda anakuweka sana pale kituoni umsubiri nawe una jinsi kumsubiri muda utakuwa umeshaenda au kuna wengine huwa wasitokee kabisa pale kituoni mwisho wa siku unaondoka na mzigo wako bila mteja kutokea.

Kuhusu kusoma vitabu, kuandika na kufanya biashara, Mara nyingi kutwa huwa nauza mashuka kuandika kwangu na kusoma vitabu ni usiku kuanzia saa 3 mpaka saa 6 au 7.. Ndani ya wiki nachagua kuandika Jumatatu mpaka Jumatano siku ya Alhamisi mpaka Jumapili ni kusoma vitabu.

Kwenye biashara yangu huwa nawashauri na wateja nawashauri wateja wasome vitabu pia. Tena nawaambia kabisa mimi ni mwandishi pia napenda kutembea na kitabu japo kimoja kwenye mkoba wangu nawahamasisha pia kusoma vitabu vya waandishi wengine.

Nikipewa mtaji nichague kati ya kutoa vitabu na kuendeleza biashara ya mashuka, nitachagua kutoa vitabu maana ni fani ninayoipenda sana pia nina imani ina faida kubwa ila tu inachokwamisha ni soko.

Ushauri wangu kwa waandishi ambao wameacha kuandika na kufanya biashara kama mimi, Wasiache kuandika maana uandishi ni fani na pia ni biashara kama tukiifanya vizuri italeta manufaa kama biashara nyingine.

Biashara yangu inapatikana Kigamboni, Mimi kwa sasa sina






ofisi ila ninafanya online kwa kutembeza ninakuletea mzigo wako mpaka ulipo... Ukurasa wetu wa Instagram ni #tatians_store ingia tufuate ujionee bidhaa zetu WhatsApp namba 0718548833.

Nawakumbusha kuwa bidhaa zangu ni nzuri sana ni pamba kabisa unapata kwa jumla na rejareja ukinunua kwetu hutoweza kujutia pesa yako. Tuna uhakika kabisa maana hatujawahi kulalamikiwa. Na wateja wetu ni wa kudumu.

Ahsante.



# Umoja ni Nguvu

## Na Hussein Mwinshehe




Salaam ndugu mashuhuda. Salaam ndugu wasomaji. Salaam wadau wote wa fasihi ya Kiswahili duniani.

Naam baada ya salaam, napenda kujitambulisha kwenu. Mimi ni yule niliyekosa la kusema na kujikuta naropoka tu. Nachoropoka wala kisikutie shaka wala kukwangua nafsi yako. Kama kimekugusa ujue kinakuhusu na kama hakijagusa jua hakijaropokwa kwa ajili yako.

Hapa sihitaji kumwomba yeyote yule msamaha maana sijakosea lolote bali nimeropoka tu. Na la mkosaji siku zote halitiliwi shaka.

Nisiwe mchoyo na mjivuni mwenye maneno mia na kenda na kusahau kichwa cha habari kinanipasa nianze kuropoka yale niliyokusudia kuyatema.

Umoja ni Nguvu. Ni kauli laini sana ambayo watunzi na waandishi wengi wameshindwa kuishi nayo na badala yake kila mmoja anatamani kwenda peke yake jambo ambalo ni nadra sana kuliona linafanikiwa kwa asilimia zote.

Wahenga wanasema ukitaka kufika nenda peke yako lakini ukitaka kufika haraka, ungana na wenzako. Ili tasnia hii ya fasihi andishi ifanikiwe, basi waandishi na watunzi pamoja na wadau wanapaswa kuungana na kulisukuma gurudumu hili zito mithili ya lile la trekta. Lakini nasikitika kwenye hili, kila mwandishi anasukuma peke yake. Kila mwandishi anataka kuthibitishia uma kuwa anaweza bila ya watu fulani. Huku ni kujidanganya kwa sababu kuna muda utahitaji kuwepo sehemu fulani ili ufanikiwe kupiga hatua zaidi.

Nimewahi kusikia hadithi ya bwana mmoja akijinadi kwa kusema yeye anaingiza milioni kadhaa kupitia uandishi. Hivyo haoni haja ya kuungana na waandishi wengine.

Yawezekana yupo sahihi kwa upande alioukalia. Yeye anaamini kuwa anaandika ili apate fedha. Lakini fedha bila kupiga hatua au fedha bila kuweka ufalme wako, ni sawa na kazi bure. Fedha huja na kuondoka lakini ufalme utabaki vizazi kwa vizazi. Kila ambaye atazaliwa, atakutaja kuwa uliwahi kuwa fulani.

Napozungumzia ufalme, namaanisha wasifu fulani ambao unauvuna kwenye uandishi. Tunashuhudia waandishi wakipata tuzo mbalimbali ndani na nje ya nchi. Tunaona waandishi wakipewa heshima za kipekee kwa sababu ya kuwa katika umoja fulani. Hizo ndizo alama ngumu kufutwa na watu.

Leo hii ukiwa Umoja wa Waandishi wa Riwaya Wenye Dira (UWARIDI) unatazamwa kwa jicho la kipekee. Jicho hilo linaweza kuwa zuri au baya lakini ni la kipekee. Hata kama litakuwa baya lakini akutazamaye anakuwa anakupa heshima na mwonekano wa tofauti kwa sababu tayari UWARIDI imejenga misingi ambayo ni ngumu kwa mtu wa kawaida kuja kuivunja.

Haya ndio mambo ya umoja ambayo yanapaswa kutazamwa kwa jicho pana na la kipekee. Tusikumbatie umimi ambao hautufikishi mahali popote. Tujitoe na kuungana kwa pamoja ili kutengeneza fasihi imara itakayokuwa urithi wa vizazi vyetu.

Tusifikie hatua ya kuwatenga hata wasomaji kisa mitazamo yetu. Tuwaunge hawa wadau na kuwapa hitaji lao. Wadau na wasomaji wanatamani sana kuona tunaungana na kuwa kitu kimoja kisha kuwapa burudani. Lakini bahati haijalala upande wao, wanajikuta wanavutwa huku na huko. Hawaelewi kwa nini wanavutwa lakini wanavutika na hadithi za wongo na kweli wanazozisikia toka kwa wavutaji.

Nisiwe mwongo, uandishi wa kisasa umejaa umimi kuliko umoja. Kila mwandishi anataka kujenga kasiri lake la fasihi bila kushirikiana na wenzake. Matokeo yake anashindwa na kuanza kulaumu watu kwa kutomsaidia. Kama umeamua kujenga kasiri peke yako, we jenga. Usilalamikie watu unapofeli. HILI NI LA MKOSAJI.

# Ni Sawa Kufanya Tendo La Ndoa Wakati Wa Ujauzito?



NA GODFREY MAKARANGA

Kumekuwa na sintofahamu nyingi kuhusu kushiriki/kufanya mapenzi wakati wa ujauzito. Kushiriki tendo wakati wa ujauzito ni Jambo la kawaida kwa wanandoa au hata wapenzi. Iwapo muhudumu wa afya ( Daktari, Muuguzi ,Mkunga nk) atakupa angalizo na tahadhari basi hakuna haja ya kufanya mbali kufuata maagizo yake.

Hii haihamasishi kufanya lakini kama mtu atajisikia kufanya au kutofanya ni maamuzi na hii inapendeza kama ujauzito hauna viashiria vyovyote vya hatari (Maendeleo mazuri ya ujauzito). Wapo wanaofanya mpaka muda mama anakaribia kujifungua na wapo ambao hawafanyi kabisa.

Wataalamu wanasema kushiriki tendo wakati wa ujauzito (Ulio salama) hakuna shida itakayotokea kwa mtoto maana maumbile ya mwanaume hayawezi kumsumbua mtoto hivyo hubaki tulii ndani ya kifuko chake (Amniotic sac') lakini pia mwanamke hutakiwi kushiriki tendo kama una ujauzito wa mapacha, Kama una historia ya kuharibika kwa mimba ,Kama una historia ya njia ya uzazi kufunguka mapema kabla ya muda na Kama unapata maumivu ya tumbo bila sababu lakini pia kama unatoka na damu bila sababu yoyote hutakiwi kushiriki tendo.

Wakati wa kufika mshindo ama kileleni kuna hali huwa inatokea ya kukaza na kuachia kwa misuli, Jambo hili huwa kawaida na haiwezi kusababisha njia kufunguka. Hivyo kama inatokea ichukuliwe kawaida.

Mtaalamu akatoa tahadhari juu ya mikao katika tendo, Hapa inaitajika mikao rafiki (Pregnancy Friendly sex positions) .

Hii mikao iliyozoeleka huwa haishauriwi kabisa maana kuna hatari ya kumsababishia matatizo kiumbe huko tumboni. Kuna mikao mbalimbali ya kukaa katika tendo na kumuacha mtoto akiwa salama huku mama akifurahia tendo. Google ipo mtatafuta hiyo mikao rafiki kwa mama na mtoto.

Kuna faida kadhaa aliongea Mtaalamu wa afya kama vile

- Mazoezi kwa mama.
- Inapunguza Maumivu kwa mama.
- Inaongeza ukaribu wa mama na mwenza.
- Mshindo huwa tofauti kwa mama na baba (Msiniulize inakuaje?)





# FUKUFUKU



## YUPO WAPI FAUSTIN MKENGE?

Wengi tulimfahamu kwa usomaji wake mahiri wa hadithi na makala mbalimbali huko mtandaoni. Alikuwa ni mchangia mada mzuri na pia alitoa sapoti kwenye mambo mbalimbali ya uandishi.

Mbali na hayo, Faustin Mkenge alipenda utani na kila aina ya vituko. Wasomaji na waandishi mbalimbali walimfahamu ndugu huyu kwa njia mbalimbali.

Lakini ni miaka sasa imepita huyu bwana kapotea mtandaoni. Haonekani tena kama zamani. Kapotea na hakuna ambaye anazungumza kuhusu kupotea kwake.

Sisi kama tulizo tayari tumemkumbuka kwa sababu ya ucheshi wake na matukio murua ambayo tuliyajenga naye. Yeyote ambaye anayejua huyu bwana alipo, ampe ujumbe wetu wa kuwa tumemkumbuka sana na ajitokeze hata mara moja na kutusalimia.

Faustin Mkenge, Tulizo Media tunakutakia kila lililo la kheri huko ulipo. Sisi kama wanafasihi wenzako tumekukumbuka sana tena sana.

# HABARI NAZI



## AMOS BWIRE, KWA MARA NYINGINE TENA

Mwandishi Amos Bwire, ambaye anatamba na kitabu cha Konstebo Mwanaidi, ameamua kuja kwa namna nyingine baada ya kuweka jalada (pichani) ambalo halina jina wala maandishi yoyote yale.

Alichofanya ni kuwapa uhuru wasomaji wake wapendekeze kichwa cha kitabu. Wadau wakajitokeza kwa wingi kumpa vichwa mbalimbali lakini mpaka sasa yupo kimya asitoe chaguo lake kwenye hili.

Za chinichini zinasema bwana huyu ambaye amebobea kwenye uandishi wa aina yake, anataka kutoa kitabu ambacho jalada lake ndilo hilo pichani. Na kitabu hicho kitakuja kabla ya mwaka kuisha.

Je, kitaitwaje? Kama ungekuwa wewe niye msomaji, ungetoa jina la kitabu lipi kupitia picha hiyo? Leta maoni yako kupitia Tulizo Media nasi tutayafikisha.

Kwa mengine mengi, mtafute facebook kwa jina la Baba BM.


TULIZO MEDIA

***TULIZO MEDIA***

*Ni Muunganiko wa Kazi Sita.*

*1. Tulizo Graphics. Kazi yake ni kufanya kazi zote za ubunifu kama vile kufanya majalada ya hadithi, riwaya, tamthiliya, nyimbo, ushairi, kupanga kitabu, kuandaa mipango ya biashara nk.*

*2. Tulizo Studio, hii ni kwa ajili ya kuandaa kazi za sauti.*

*3. Tulizo Magazine. Hili ni jarida linaloruka kila mwezi.*

*4.Tulizo Printing. Kazi yake ni kuchapa kazi mbalimbali.*

*5. Tulizoflix. Huu ni ulimwengu wa filamu ambapo tulizo huzichambua.*

*6Tulizo Visual. Hapa ni kwenye kutengeneza videos na kupiga picha mbalimbali zenye viwango.*

***Kwa huduma wasiliana nasi kwa +255 627 585 638***

# 3 KALI ZA OKTOBA

## 1

### MALKIA WA UZURI

**Riwaya ya mwanadada Agnes Mgoji ambayo inaelezea mapito ya binti Makena aliyepitia changamoto za manyanyaso na ukatili wa kijinsia.**

**Kitabu hiki kitazinduliwa siku ya tarehe 12. Novemba. 2022 katika shule ya sekondari Kawe, Jijini Dar es Salaam**

## 2

### BILA HURUMA


**PETER SHAYO**
**Mwandishi wa Mashairi ambaye kaamua kujitosa kwenye upande wa riwaya pia. Amekuletea kitabu cha Bila Huruma ambacho nacho kinaelezea kinaga ubaga kuhusu manyanyaso na ukatili dhidi ya wanawake.**


**Ni kitabu mahususi kwa jamii ya sasa. kitafute.**


## 3

### MWIMBULA

**FRANK MASAI**
**Ni kitabu kingine ambacho nacho kinaelezea matatizo mbalimbali ambayo wanawake wanayapitia. Ni kitabu kinachokumbusha kuhusu mila na desturi za Mwafrika. Pia kinaangazia masuala ya unyanyasaji wa kijinsia na njia kadhaa ya kuyatatua. Kinapatikana. KITAFUTE.**











# Makange ya Kuku

**Sophia Hamad**

**Kwa Watu Wanne**

## Mahitaji

*1.Kuku mmoja*
*2.Mafuta ya kupikia Lita 1*
*3.Vitunguu Swaumu viwili*
*4.Kitunguu Maji kikubwa kimoja*
*5.Tangawizi iliyotwangwa (kulainishia nyama ya kuku)*
*6.Pilipili hoho 2 Karoti 4*
*7.Pilipili mbuzi au pilipili ndefu 1 (ukipenda kama unatumia)*
*8.Chumvi, Ndimu au Limao*
*9.Nyanya fresh 2*
*10.Tomato paste kijiko kikubwa cha chakula 1*
*11.Chicken Masala*

## Hatua za Mapishi:

*1.Tengeneza kuku. Muoshe vizuri, mkatekate vipande vidogo vidogo.*
*2.Mpake Kitunguu Swaumu na tangawizi zilizotwangwa, kamulia ndimu au limao. Weka chumvi na chicken masala.*
*3.Mwache kwa muda viungo vimuingie vizuri.*
*4.Kata vipande vikubwa vya pilipili hoho, vitunguu na karoti. twanga na Kitunguu swaumu cha pili kwa ajili ya kukaangia makange.*
*5.Saga nyanya zako zihifadhi, washa jiko la kupikia.*
*6.Weka mafuta kwenye karai.vAcha yachemke kabisa.*
*7.Mtoe kuku ulipomhifadhi anza kukaanga vipande vyake mpaka viive.*
*8.Vipande vya kuku vyote vikishakaangwa na kuiva vihifadhi pembeni acha vipoe kidogo.*
*9.Punguza mafuta kwenye karai ya kukaangia.*
*10.Anza kukaanga viungo vya Kitunguu maji na Kitunguu swaumu, kisha kaanga karoti na pilipili hoho.*
*Hivi viungo vya karoti na pilipili hoho visiive sana, vinatakiwa vibaki vionekane kwenye makange.*
*11.Weka nyanya zako fresh, ongeza na tomato paste.*
*kaanga kidogo, anza kuweka vipande vya kuku aliyekaangwa kwenye viungo unavyokaanga.Koroga na geuza upawa wako mara kadhaa kuhakikisha viungo hivyo vimekaukia kwenye vipande vya kuku (isiwepo rosti,kama kwenye mchuzi).*
*Ukiona hivyo ipua, makange yapo tayari kutowelea chakula chochote upendacho iwe ni ugali, chapati, au ndizi choma.*



# ULIMWENGU WA TULIZO



Yupo mwanzilishi wa tatu wa kampuni ya apple. Huyu aliuza 10% ya shea zake kwa dola 800. Leo shea hizo ni dola bilioni 35



Ukijaribu kujiua Korea Kaskazini, hauendi jela peke yako. Watoto na wajukuu zako pia watakwenda na wewe.



Huko Taiwan, kuna jamaa aliamka kutoka kwenye coma baada ya kutajiwa chakula anachokipenda.




Da Vinci alitumia miaka kumi na mbili kumaliza kuchora lips za Monalisa (Pichani)



Huko Italia kuiba chakula si kosa kama chakula hiko kimeibwa na masikini au mtu mwenye njaa.



1962 kulikuwa na pendekezo la kuibadili Ufilipino kuwa Malaysia. Ila nchi jirani wakalichukua pendekezo lao halijapita



Switzerland, kwenye kumbi za kuonyesha filamu kuna TV hadi chooni ili mtu asipitwe na filamu inayoonyeshwa.




Ni kosa la jinai huko Singapore kutoflashi choo baada ya kujisaidia haja zako.



Katika kisiwa cha Maldives, hakuna nyoka wala wadudu wenye sumu.



Michael Jordani hupokea pesa nyingi toka Nike kuliko wafanyakazi wote wa kiwanda cha Nike cha Malaysia.




2006, CNN waliwaweka Mark Zuckerberg na mwanzilishi wa Netflix kwenye list ya watu kumi wa kupuuzwa.



Mbwa wanafahamu binadamu hawana uwezo mkubwa wa kuona gizani hivyo hupenda kuiba chakula gizani.

# NENO LA TULIZO

## VITA YA MAISHA

## ENOCK - DODOMA

Inaweza kukufanya uwapoteze watu muhimu walioibeba sehemu ya thamani ya maisha yako, jitafakari.

Inaweza kukuweka katika ulimwengu usiokuwa na binadamu yeyote wa kukukumbusha mahali ulipo mlango wa mafanikio ulioamua kuupa mgongo, usiogope kugeuka kwa dhumuni chanya.

Inaweza kukupa kiburi na kusahau kuwa dua zetu tunazoziomba kila siku hujibiwa na MUNGU kupitia watu ulioamua kukaa nao mbali, acha kujikweza.

Inaweza kukuweka katika mapambano lakini usijue njia sahihi ya kupambania, punguza ujuaji.

Ni vita ya maisha.

Haiitaji hasira, jazba na sifa kama za Mandonga kuwa yakikupiga ni sawa na umeyapiga. Yakikupiga ikubali changamoto, jifunze ulipokosea, kisha endelea.

Nakudokeza;

Usikubali kuwa mpambe wa vita ya maisha yako au usubiri mshenga wako ndio amvalishe pete ya harusi mkeo mtarajiwa, umeliwa.

Hakuna atakayekuja kukunyanyua bila wewe kukubali kunyanyuka kwanza, pambana.

Haiitaji watu wababe waliopenda kukaa *backbencher* kule shuleni. Darasa la huku nje halina mtu wa kukukumbusha usogee katika kiti cha mbele zaidi yako. Amka kwenye hiyo ndoto yako.Ndoto itaendelea kuwa ndoto ukiendelea kulala, inahitaji uamke na uisimulie kwa vitendo, kisha uache mdomo umsimulie Mola wako sifa zake.

"Hope is a start but hope needs action to win victories." Anasema David Schwartz.

Wakikushauri kwa miluzi yao, usiihukumu kuwa humpoteza mbwa, ichague inayoweza kuwa silaha nzuri kwako. Itumie ikufaapo.

Kumbuka;
Haina uhusiano wowote na kukaa ndani au kushinda vijiweni kuzipiga soga huku ukisukumwa na upepo wa "SISI NDIO TUNAOSAIDIWA NA BWANA". Au hujui kuwa imeandikwa tafuteni nanyi mtapata?

Inuka uangaze kwa kuwa nuru yako imekujia, imeandikwa katika kitabu cha Isaya.

Enock
27/10/22
Dodoma




## *Mpigie Kura Yusta Lucas*

Akiwa ni miongoni mwa waandishi wachache waliojiajiri, Binti Yustar Lucas anakuja kwenu wadau a wasomaji wa Jarida la Tulizo na kuomba mumpigie kura ili aweze kushinda tuzo ya mwanzilishi bora wa biashara.

Kupiga kura ni rahisi sana, ingia kwenye wavuti ya ***www.youngceort.co.tz*** kisha ingia upande wa business START UP. Utaona picha hii ya kushoto kwako na chini kuna kiduara kidogo. Bonyeza kiduara hicho kisha shuka hadi chini na kupiga kura.

Kama huna akaunti, bonyeza create new account kisha weka email na majina unayoyatumia. Rudi na kumpigia kura Yustar Lucas.

# TULIZO SPESHO

# MREMBO NA MNYAMA

## CHRISTINE BELLINGTON

Hapo zamani za kale katika nchi ya mbali aliishi Mfanyabiashara tajiri na mabinti zake watatu.
Yule wa tatu alikua mzuri na mwenye busara zaidi kushinda wenzake hivyo kila mmoja alimwita Mrembo. Kwa upande mwingine dada zake walikua wenye vivu na wasio na busara, walivutiwa zaidi kutumia pesa za baba yao.

Mrembo alikua akiota kuhusu Mwanamfalme nadhifu siku zote, aliamini ya kuwa iko siku ataolewa na Mwanamfalme na kuishi nae katika kasri ya kuvutia.
Kila kitu kilikua cha furaha katika maisha ya Mrembo kama ilivyo ndoto yake.

Pasipo kutarajia tumaini lake lilipotea. Ilitokea dhoruba kubwa iliyoangamiza meli zote za baba yake pamoja na utajiri wake wote.

Baba alirejea nyumbani mwenye huzuri akawaeleza binti zake.

"Usijali baba kila kitu kitakua sawa punde tu tutapata namna nyingine. Wewe ndio utajiri wangu pekee, nina furaha kuwa nawe. " Mrembo alisema.

Muda haukupita sana vijakazi wote waliondoka pale nyumbani sababu ya umasikini. Mrembo alichukua majukumu ya nyumbani wakati dada zake wawili wakimlalamikia baba yao kwa umasikini uliopo nyumbani pale.

Mrembo siku zote alimwomba Mungu kuirudisha furaha katika uso wa baba yake. Haikuchukua muda sana yule Mfanyabiashara alipokea habari ya kuwa moja kati ya meli zake imetia nanga bandarini.

"Nina habari nzuri moja kati ya meli zangu imetia nanga bandarini, hatutaishi fukara tena. Muda ndio huu inabidi mniambie kila mmoja niwaletee zawadi gani?" Baba alisema.

Binti wa kwanza alijibu anataka mavazi mapya, wa pili aliagiza vito vya thamani. Lakini Mrembo alijibu," ninachotaka ni wewe kurudi nyumbani salama."
Baba alisisitiza ndipo Mrembo akamwomba amletee uwaridi moja tu.

Kwa taarifa ile ya kuvutia Mfanyabiashara alifunga safari kuelekea bandarini. Alipofika alikuta meli imetelekezwa na wahudumu wote wametoroka na mizigo iliyosalia.

Akiwa amevunjika moyo na mwenye mawazo mengi alianza kurudi kuelekea nyumbani. Mara alipotea njia na kuingia katika msitu mnene. Theluji ilikua ikidondoka kana kwamba bahari yote imegeuka barafu. Farasi alishindwa kuendelea kutembea kwa wingi wa barafu. Mfanyabiashara alishuka juu ya farasi.

Kwa mbali aliona mwanga na kuanza kuufuata. Ilikua ni kasri kubwa ya kuvutia. Alipofikia lango lililopambwa kwa dhahabu lilifunguka. Ilikua ni ajabu kuwa hapakua na barafu iliyodondoka katika eneo la miti ya machungwa ya kuvutia.

Alidhamiria kuingia ndani ili akaombe msaada kwa Mfalme wa wa kasri lile. Alipita katika bwalo kubwa, akasimama na kutizama huku na kule kama kuna mtu angekuja lakini baada ya kusubiri kwa muda hakutokea mtu.

Alijaribu kubisha hodi pia ila hakuitikia yeyote. Palikua na meza iliyojaa vyakula vizuri, keki za kuvutia na matunda. Aliketi akaanza kula.

Hakupoteza muda kwa kula punde tu alimaliza. Alipanda ngazi kuelekea juu. Alifungua mlango na kuona chumba kizuri chenye kitanda nadhifu akalala.

Asubuhi ilifika, akafumbua macho yake na kuona ni siku nyingine tena angavu.
Alikuta mavazi mapya tayari kwa ajili yake, alijiandaa na kushuka chini katika bwalo.

Chakula cha asubuhi kilikua tayari mezani. Maziwa, maji ya matunda na mikate. Alikula kiasi chake. Alipomaliza aliinuka na kumshukuru mwenyeji wake hewa kwa sauti ya juu kisha alitoka nje ya kasri tayari kwa kuondoka.

Wakati anatoka aliyaona maua mengi kiasi cha kushangaza yakiwemo mauwaridi. Alikumbuka ombi la binti yake mrembo na kuelekea bustani ilipo na kuchuma ua moja.

Punde tu alipochuma ua palitokea sauti ya kutisha nyuma yake, ardhi ilirindima kufuatia kishindo kikubwa, aliogopa sana. Alipogeuka alijikuta amesimama mbele ya mnyama mkubwa mwenye macho mekundu mithili ya damu, meno marefu na kucha zake mithili ya visu vikali.

ITAENDELEA

# MTEGO WA KIFO

NELSON NTIMBA
+255 556 353 765

Ishu yenyewe ilianza asubuhi ya Jumatano moja ya mwezi saba, msimu wa kiangazi - wakati anga zinapozokosa dalili yeyote ya mvua hivyo kusababisha vumbi linalokera.

Kwenye makutano ya barabara ya Fort Scott na barabara ya Nevada, kumejengwa sheli ambayo ina mgahawa mzuri wa kupatia chakula: Aina ya migahawa ambayo utaikuta kila palipo na sheli. Mgahawa ulikuwa umejengwa kwa mbao na ulikuwa unamilikiwa na mwanamke mmoja mjane ambaye alishirikiana na binti yake wa kike kuuendesha.

Gari ndogo aina ya Packard iliegeshwa nje ya mgahawa huo dakika chache kabla ya kuhitimu saa saba kamili za mchana. Kulikuwa na wanaume wawili ndani ya gari lenyewe. Mmoja alikuwa macho na mwingine alikuwa amelala. Dereva, ambaye alijulikana kwa jina la Baro, mwanamume mfupi, mnene mwenye uso uliojaa nyamanyama na kovu kubwa juu ya midomo yake alishuka kutoka kwenye ile gari. Suti aliyokuwa amevaa ilikuwa imepauka na nyuzi zilizoishikilia karibu zilikuwa zinaenda kukata tamaa kubeba nyamanyama za Baro. Shati alilokuwa amevaa lilikuwa ni chafu nalo halikumuenea vizuri. Alikuwa anajisikia vibaya. Usiku wa jana alikunywa sana pombe na ukali wa jua ndiyo ulimsababishia ajihisi vibaya zaidi.

Alisita kwanza na kumuangalia mwenzake ambaye alikuwa amelala, Sam, halafu akaguna na kuelekea eneo la mgahawa ule akimuacha Sam akiwa anakoroma ndani ya gari.

Alipoingia mgahawani, binti aliyekuwa anasafisha meza za mule ndani aliachia tabasamu. Yule binti alikuwa na meno ya kuvutia. Meupe yasiyokera kuangalia. Hata hivyo, kuna kitu hakikumvutia Baro kuhusu binti huyu. alikuwa mnene sana. Hivyo Baro hakurudisha tabasamu.

"Habari yako, kaka!" Yule msichana alimsalimia Baro kwa uchangamfu na kuongeza, "Kuna joto kweli. Kama jana usiku sijalala kabisa."
"Naomba Scotch," Baro alijibu kwa ufupi tu. Halafu akaisogeza kofia yake nyuma kidogo na kutoa leso mfukoni na kujifuta uso wake uliokuwa unatiririka jasho.

Yule msichana aliweka chupa ya Scotch na glasi mezani.

"Unatakiwa unywe bia," Alisema. "Pombe kali sio nzuri haswa kipindi hiki cha kiangazai."

"Upumzishe mdomo wako," Baro alijibu. Halafu akabeba glasi na ile chupa ya Whisky na kuendea meza iliyokuwa kwenye kona kuketi huko peke yake.

Yule msichana alibaki anamtazama tu kwa jicho la mshangao kabla hajaamua kuendelea na shughuli zingine.

Baro alipiga fundo moja kubwa, halafu akaegemea kiti alichokuwa amekalia. Mawazo yake yote yalikuwa kwenye pesa. Kama Frank asipokuja wazo la kutupatia pesa mapema, basi itatulazimu tuvavamie benki. Alijigunia. Hakuwa anataka kufikia uamuzi huo. Kipindi hiki askari walikuwa wamechachamaa. Alitupa macho yake nje ya dirisha na kumuona Mjomba Sam akiwa bado kalala. Baro akafyonza. Ukitoa ujuzi wa kuendesha gari, Sam alikuwa hana msaada wowote tena, Bailey alijiambia. Huyu amekwisha zeeka kujihusisha na shughuli za aina hii. Kitu pekee anachowaza ni kula na kulala tu. Hivyo ni jukumu langu mimi na Frank tuhakikishe tunapata hela – lakini tunapataje hizo hela?

Whisky ilianza kumpa njaa.

"Naomba mayai na mkate," Baro Alimwambia yule msichana wa mapokezi.

"Na yule aliyelala na mpelekea?" Yule msichana aliuliza huku akimuoneshea Mjomba Sam.

"Unavoona ni kama anahitaji chakula yule." Baro alifoka. "Harakisha kuniletea hiko chakula. Nina njaa."

Akiwa anasubiria chakula chake, kupitia dirishani aliona gari aina ya Ford ikiegeshwa na mwanamume mmoja mzee alishuka kutoka kwenye ile gari.

Henry! Baro alijisemea, Amekuja kufanya nini hapa.
Yule mwanamume aliingia ndani ya mgahawa na kumpungia mkono wa salamu Baro.

"Mambo vipi?" Henry alisema. "Muda mrefu hatujaonana, mambo yanasemaje?"

"Mambo sio mambo," Baro alilalamika. "Hili joto linaharibu kila kitu."

Henry alisogea karibu. Akavuta kiti na kuketi. Huyu jamaa alikuwa anafanyia kazi kundi moja la utapeli na yeye alikuwa ni mtu wa kukusanya taarifa hapa na pale – hivyo alikuwa anafahamu mambo mengi ambayo yalikuwa yanaendelea mjini hapo. Alikuwa na taarifa za hapa na pale ambazo zingepelekea utekaji nyara hadi mauaji kwa Kansas yote.

"Unaweza kurudia kusema hivyo tena," Henry alisema. "Nilikuwa nipo Joslin usiku wa jana kwenye harusi nikahisi kama nakaangwa kwa lile joto." Alipomtazama Baro aligundua hakuwa akimsikiliza. Akaongeza swali, "Vipi. Mbona unaonekana una huzuni."

"Nina hali mbaya kwa wiki kadhaa sasa." Baro alisema huku akituma chini kishungi cha sigara.

"Vipi, nikupe tip?" Baro alisema. "Anza kubeti."

Yule msichana alifika na kukatisha maongezi yao akiwa kabeba sahani ya mayai na mikate. Henry alitolea macho ile sahani ikiwa inawekwa mezani.

"Na mimi niletee hivihivi, mrembo." Henry alisema. "Leta na bia moja." Yule msicha alitoa tabasamu na kuondoka kuelekea ilipo meza ya mapokezi.

"Hiyo ndiyo aina ya wanawake ninayopenda. Halali kabisa kutumia kiasi chochote kwa mwanamke huyo." Henry alimtazama tena yule msichana. Lakini Baro akamstua. "Nina uhitaji na hela, Henry. Una wazo lolote?"

"Sijasikia jambo lolote. Ikitokea nimesikia nitakushtua, ila kwa sasa kazi zote nilizonazo ni kubwa kukushinda. Na usiku wa leo nina kazi kubwa. Nitakuwepo kwenye sherehe ya binti wa Mariki. Kiingilio elfu ishirini ila vinywaji bure."

"Mariki? Ndiyo nani?"

"Umekuwa ukiishi wapi?" Henry aliongea kwa kukereka kidogo. "Mariki ni huyu jamaa tajiri hapa mjini pote. Wanasema ana utajiri wa mabilioni ya mkwanja."

Baro aliangusha yai lake kwa habari ile.

"Na mimi utajiri wangu ni elfu kumi tu!" Baro alisema na kuongeza, "Ndiyo maisha. Kwahivyo kuna habari ipi kumhusu?"

"Sio habari kuhus yeye: Ni kuhusu binti yake. Umewahi kumuona? Mrembo! Nipo tayari nikatwe miaka kumi ya kuishi kwenye uhai wangu ili anikumbatie tu."

Baro hakujali sana maelezo hayo. "Sasa baba yake anamfanyia hafla; ni siku yake ya kuzaliwa ya ishirini na nne- umri sahihi kabisa. Inasemekana baba yake leo atamgawia binti yake mkufu wa thamani sana wa almasi. Wanasema mkufu ule unagharimu kama milioni sabini na tano."

Yule mhudumu alifika na chakula cha Henry na kukikalisha mezani. Alipoondoka, Henry alisogeza kiti na kuanza kula kwa fujo. Baro alikuwa amemaliza kula. Alikuwa anachokonoa meno huku kichwani kwake akifikiria; Milioni sabini na tano. Sijui kuna namna ya kuupokonya huo mkufu? Sijui kama Frank ataweza kuwa na ujasiri!

"Kwani sherehe yenyewe inafanyikia wapi? Nyumbani kwao?"

"Ndiyo." Henry alisema, huku akijaza chakula mdomoni. "Halafu wakitoka hapo yeye na bwana wake wanaelekea hoteli ya Golden Slipper Roadhouse."

"Wanaenda na huo mkufu?" Baro aliuliza kwa umakini akiyachunga maneno yake.

"Nadhani pindi atakapouning'iniza shingoni hatouvua tena."

"Ila hauna uhakika?"

"Si lazima atauvaa tu, au? Basi hatouvua huo mkufu."

"Kwani huko Roadhouse anaenda saa ngapi?"

"Majira ya saa sita usiku, sherehe iki.." Henry hakumaliza kauli yake, akaganda na chakula kikiwa kimekaribia kuingia mdomoni. "Unawaza nini?"

"Siwazi kitu."

"Kwahivyo usiku wakiondoka kwenye sherehe watakuwa ni wao wawili tu?" Baro aliendeleza udadisi.

"Ndiyo!" Henry alijibu. Uso wake ulikuwa na wasiwasi. "Sasa sikia, usianze kupanga mipango humo kichwani mwako. Unaweza kujikuta umeanzisha jambo ambalo hauwezi kulimaliza. Wewe na Riley hamuwezi kufanya hiyo kazi. Kwahivyo kuwa mvumilivu kuna kazi nitakutafutia, ila huo mkufu achana nao!"

Baro aliguna. "Usinipe ushauri." Alisema, "Ninafahamu kipi naweza kufanya na kipi siwezi." Baro akasimama. "Naona niondoke. Na usisahau ikitokea kuna jambo lolote la kuingiza hela nistue. Kwaheri."
"Mbona umekuwa na haraka ghafla?" Henry alisema.

"Ninataka niondoke kabla Mjomba Sama hajaamka. Sina hela ya kumnunulia chakula akistuka na kunikuta nipo humu."

**ITAENDELEA**

# HADITHI: BELLA

SAFINA SALIMU
+255 623 398 039

Ilikua saa 8:00 mchana, Bella akiwa nyumbani kwa wazazi wake, hakuna achofanya, ameshafanya shughuli zake amemaliza.

Mama akitoka chumbani kwake kuelekea sebuleni akiita, "Bella..."
Bella alinyamaza. Mama akamuita tena "Bella."

*(Bella akinung'unika)* mama na wewe, unaniita nini? Nishafanya shughuli zangu, nimeshamaliza.

**Mama**: Kwa hiyo, n'sikuite? Kwanini wewe ni nani? Hapa ni kwangu, hata kama wewe, ushakua mtu mzima. Na kama unajiona mtu mzima ondoka. Kazi hutaki kwenda kutafuta, upo tu hapa nyumbani, miaka 22 bado unategemea n'kulishe. Halafu nakuita unanyamaza.

**Bella:** Sasa mama mimi n'tafanya kazi gani? Nataka n'kasomee kazi ya hoteli, mimi kazi za kuhangaika siwezi kabisa.

**Mama**: Kwani aliyekuambia, kazi za hoteli ni za kukaa nani? Yaani kama hujasoma, hujasoma tu, lazima maisha yako yote uhangaike. Ukitaka utegemee mwanaume, utakua mtumwa mpaka unakufa. Wakati una nafasi ya kusoma, ulikua unajifanya husikii, ukajiona binti mzuri, mtaa mzima hakuna. Ukipita barabarani wanaume wanakusifia, unajiona cake. Sasa hivi n'do unajuta. Mwenzako Lisa yupo chuo sasa hivi, wewe kwanza na kuzeeka, utazeeka mapema, maisha ya kubangaiza magumu sana. Tena zama zenu hizi, mna kazi maana maisha ya sasa hivi yamekua magumu sana. Mambo yamebadilika, ukitaka kuolewa, uwe wa kupewa tu, utateseka mpaka utaamua utoke. Utaenda kutembeza machungwa barabarani. Naona bado kuna watu, wanakutumia visenti, nd'o vinavyokuchanganya.

*(Mama yake, akiwa anatoka nje)* Mi naenda. Saa mbili chakula kiwe tayari kwa sababu baba yako, akirudi atakua na njaa.

**Bella**: *(akiwa anarudi ndani ,simu yake ikiwa inaita akaipokea)* haloo! Baby, naomba n'saidie elfu tano, nilikua na shida.

*(Huyo bwana anaitwa Kassim)*

**Kassim**: Sawa, nitakutumia baadaye. Akakata simu.
*(Kassim akawa analalamika)* Mimi mwenyewe, maisha yangu magumu. Halafu nimtumie elfu tano, halafu hiyo elfu tano, utasikia, baby, tuma na ya kutolea)

**Bella**: Nitumie kwa namba hiihii.

**Kassim**: (akicheka) Akamtumia ujumbe. *katafute kazi, mi sina hela.*

**Bella**: *(akaanza kulia)* yaani huyu mwanzoni, alikua ananitumia hela, sasa hivi elfu tano tu, anakataa. Ngoja nimtafute Yusuph.

(*akitafuta namba kwenye simu akaipata)*

**Bella**: hallo baby!! naomba nisaidie elfu kumi. Yusuph yeye akamtumia hapohapo.

**Bella**: *(Akashukuru kwa ujumbe)* Sasa hapa, ngoja nipige picha, nimtumie editor. Anifanye kama nipo hoteli hivi nakula bata. Akaunga kifurushi cha data, akaanza kujiweka mtandaoni.

*Lisa, yule jirani yake, akamuona mtandaoni.*

*{Lisa akamtumia ujumbe)* Shoga hongera, sasa hivi naona, unakula bata.

**Bella**: Ndio shosti, nipo napunga upepo wa Zanzibar, si unajua maisha yenyewe, mafupi haya?

**Lisa:** Hongera sana, mi nipo chuo, nd'o nakaribia kumaliza chuo.

**Bella**: (akinyanyuka kitandani) poa nyie wasomi, endeleeni kuteseka, sisi hatujasoma lakini tunakula bata.

LISA: *(kwa unyonge)* sawa, yote maisha.
*(Lisa akiongea mwenyewe, hivi haya maisha yako vipi, yaani sisi tunahangaika na kukesha tukisoma, mwenzetu juzi tu, kishakua na maisha mazuri)*

Ilivyofika saa mbili, nd'o Bella anatoka anaenda kupika, akiwa anawasha moto.

**Mama**: *(akirudi kutoka kwa jirani, akiwa nje)* Bella, chakula tayari? *(akiingia jikoni)*

*(Akashika mdomo kwa mshtuko)* ndo unawasha moto? Na muda wote, ulikua unafanya nini? nikianza kuongea hapa, unione mbaya. Hapa ni kwangu, naomba utii maelekezo ya nyumbani kwangu, kama unajiona umekua mtu mzima, ondoka nenda kajitegemee, ili ufanye utakavyo.

**ITAENDELEA**

# Nyota ya Lulu

Otieno Mjomba

